

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**  
**WIZARA YA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI**

Simu: +255-26-2323201-7  
Nukushi: +255-26-2323208  
Barua pepe: [nje@nje.go.tz](mailto:nje@nje.go.tz)  
Tovuti: [www.foreign.go.tz](http://www.foreign.go.tz)



Mji wa Serikali,  
Mtumba,  
S.L.P. 2933,  
40466 DODOMA.

**TAARIFA KWA UMMA**  
**WATANZANIA WALIOPO NCHINI ISRAEL**  
**KUREJESHA NYUMBANI**

**Dodoma, 14 Oktoba 2023**

Kufuatia kuendelea kuzorota kwa hali ya usalama nchini Israel na maeneo mengine ya jirani, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeandaa mpango wa kuwarejesha nchini Watanzania waliopo nchini humo na maeneo mengine ya karibu. Serikali imefikia uamuzi huo baada ya kufanya tathmini na kujiridhisha kwamba mazingira ya sasa yanaruhusu zoezi hilo kufanyika.

Hivyo, Watanzania walio tayari kurejea nyumbani wanashauriwa kujiandikisha kwenye Ubalozi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania uliopo Tel Aviv, Israel kupitia barua pepe: [telaviv@nje.go.tz](mailto:telaviv@nje.go.tz) au simu namba: +972 533 044 978 na +972 507 650 072, kabla ya tarehe 15 Oktoba 2023, saa 6 usiku.

Imetolewa na Kitengo cha Mawasiliano Serikalini  
**WIZARA YA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA**  
**MASHARIKI**